**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI**
**SHULE YA SEKONDARI MOHORO,**

S.L.P 80,
IKWIRIRI/RUFIJI.
SIMU: 0757 106 740 / 0628 603 604.
E-mail: *mpela.sb@gmail.com*

KUMB.NA: MOHSS/F.V/2022/…… TAREHE: 07/04/2022

MZAZI/MLEZI WA:…………………………………………………………………….……….
KUTOKA SHULE YA MSINGI………………………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO – 2022/2023**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba kijana wako (mtajwa hapo juu) amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mohoro mwaka 2022 kwa mchepuo wa……….. Tunampongeza sana kwa hatua hii ya mafanikio.

Shule hii ni ya Bweni (Boarding School) kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita na ina nafasi za hosteli kwa wasichana na wavulana wa madarasa ya chini (kidato cha kwanza mpaka cha nne).

Shule ya Sekondari Mohoro ipo katika kijiji cha MOHORO kata ya Mohoro, Wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani. Mohoro ipo takribani umbali wa kilomita 207 kutoka Dar Es Salaam ukielekea barabara ya mikoa ya kusini. Kwa wanafunzi wanaotokea mikoa ya kusini LINDI na MTWARA washuke MOHORO kituo cha GOGOZEMBE na kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike DAR ES SALAAM-MBAGALA RANGI TATU ndipo watapata mabasi yanayokuja MOHORO moja kwa mmoja. Nauli ya abiria kutoka DAR ES SALAAM kuja MOHORO ni shilingi elfu saba (7,000) tu.

Muhula wa masomo utaanza tarehe……………………. hivyo anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe hiyo………….. na mwisho wa kuripoti ni tarehe………………. ***Tafadhali asicheleweshwe ili aweze kufanya vizuri katika masomo yake.*** Ikiwa kuna sababu yoyote isiyokwepeka itakayopelekea kuchelewa shule au ukiamua kumpeleka shule binafsi toa taarifa ya maandishi mapema kwa MKUU WA SHULE kupitia namba za simu na e mail ya hapo juu kabla ya tarehe ya kufungua shule ili kuepusha usumbufu kwako, shule au kwa serikali.

NB: Mwanao atapokelewa shuleni iwapo yeye na wewe mtayasoma maelekezo, kuyakubali na kujaza maelezo yote yaliyomo katika viambata A – F

A. Maelezo maalum ya kujiunga na shule
B. Ada na michango mbalimbali ya shule
C. Sheria, kanuni na taratibu za shule
D. Vitabu na vifaa vya usafi
E. Fomu ya vipimo vya afya kwa mwanafunzi (Medical Examination Form).

"KILA WAKATI FIKIRI KWANZA KABLA YA KUNENA NA TUMIA BUSARA KABLA YA KUTENDA…KILA MMOJA ATIMIZE WAJIBU WAKE"

Nakutakia maandalizi mema
Wako

……………………
SALUM B MPELA
MKUU WA SHULE

A. <u>MAELEZO MAALUM YA KUJIUNGA NA SHULE</u>

I. SARE ZA SHULE:

- Shati mikono mifupi au nusu kanzu mikono mirefu - (rangi nyeupe) mbili.
  NB: Nusu kanzu ifunike makalio na ivaliwe na ushungi (hijab) nyeupe inayofunika hadi kifuani na iwe ya kupwaya (isibane mwili).
- Sketi mbili rangi ya **kijani jeshi** ndefu na ivuke magoti inch 5 au zaidi kwa kwenda chini, mshono wa rinda box.
- Sketi rangi **ya udongo (rangi kama ya sare ya jeshi la magereza)** kwa ajili ya kushindia na zitavaliwa baada ya vipindi vya darasani.
- Soksi ndefu **NYEUPE** jozi mbili au zaidi.
- Viatu **VYEUSI VYA NGOZI** viwe na visigino vifupi, vya kufunga na kamba na visivyokuwa na urembo wowote. Vibajaji na ndala HAVIRUHUSIWI.
- Raba nyeupe za michezo na fatiki jozi moja
- Fulana za michezo jezi ya Taifa Stars rangi nyeupe
- Mitandio ya kushindia ya rangi ya bluu bahari (kwa wanaotaka)
- Fulana ya kushindia zenye nembo ya shule (zinapatikana jirani na shule)
- Sweta la rangi ya kijani jeshi
- Jezi za michezo (TRACKSUIT YA BLUU BAHARI NA FULANA YA BLUU BAHARI)
- Kandambili kwa ajili ya kuogea

N.B: Mwanafunzi awe amevaa sare wakati wa kuripoti na wakati wa kwenda nyumbani

**II.** VIFAA VYA KUJIFUNZIA:

Daftari kubwa 08 au zaidi (counter books Q2 au Q3)
Kalamu /penseli za kutosha
Mkebe wa vifaa vya hesabu
Kamusi (English-English Dictionary) ya OXFORD na
Dissecting kit kwa wanafunzi wa mchepuo wa CBG
Scientific calculator kwa wanafunzi wa chepuo wa CBG
Koti jeupe la maabara mikono mifupi-urefu lifike magotini kwa mkondo wa CBG
Begi kwa ajili ya kubebea vifaa vyake vya kujifunzia.

III. MAHITAJI YA BWENI

- Godoro la futi 2.5 kwa 6
- Shuka tatu rangi ya bluu bahari
- Mto na foronya mbili rangi ya bluu bahari
- Sabuni, taulo, mswaki na dawa ya meno
- Nguo za ndani (chupi 12 au zaidi)
- Ndoo mbili za lita 10
- Sanduku imara la bati (tranka) moja lenye makufuri mawili
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe, kijiko, chupa ya chai)

IV. MAHITAJI MENGINE

- Picha sita (06) za passport size akiwa amevaa shati jeupe na rangi ya bluu nyuma
- Rimu moja ya karatasi A4 kwa mwaka
- Result slip ya kidato cha nne (CSEE) halisi na nakala
- Cheti cha kuzaliwa halisi na nakala
- Picha mbili za wazazi au/na walezi watakaoruhusiwa kuja kukutembelea (ppt size)
- Kadi ya bima ya afya NHIF au CHF au yoyote inayokubalika kituo cha afya
- Jembe lenye mpini na fyekeo - CBG
- Ufagio laini, panga na fyekeo - HGL
- Ufagio mgumu, mopa na sqweezer - HGK

**NB:** Gharama ya usafiri na matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

B. ADA NA MICHANGO

| S/N | MALIPO | KIDATO CHA TANO | | KIDATO CHA SITA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MUHULA 1 | MUHULA 2 | MUHULA 1 | MUHULA 2 |
| 1 | ADA (KARO) | 35,000 | 35,000 | 35,000 | 35,000 |
| 2 | TAALUMA | 20,000 | - | 20,000 | - |
| 3 | TAHADHALI | 5,000 | - | 5,000 | - |
| 4 | UKARABATI | 15,000 | - | 15,000 | - |
| 5 | ULINZI/MATRON/UPISHI | 30,000 | - | 30,000 | - |
| 6 | HUDUMA YA KWANZA | 10,000 | - | 5,000 | 5,000 |
| 7 | MTIHANI WA NECTA | - | - | 50,000 | - |
| 8 | MTIHANI WA MOCK | - | 20,000 | 20,000 | - |
| 9 | MTIHANI WA PRE-NECTA | - | - | - | 10,000 |
| 10 | KITAMBULISHO | 6,000 | - | - | - |
| 11 | NEMBO YA SHULE | 2,000 | - | - | - |
| | **JUMLA NDOGO** | **123,000** | **55,000** | **180,000** | **50,000** |
| | **JUMLA KUU** | **178,000** | | **230,000** | |

**N.B:** MALIPO YOTE YALIPWE KUPITIA BENKI YA NMB, AKAUNTI YA SHULE NAMBA 21301100053 JINA LA AKAUNTI NI: MOHORO SECONDARY SCHOOL-RECURRENT. Wakati unafanya malipo hakikisha unatumia jina kamili la mwanafunzi kama ni jina la MLIPAJI. Aje na risiti (pay-in-slip) ya malipo anaporipoti shuleni. Ukilipa kwa wakala wa NMB ambatanisha na risiti ya mashine ya EFD. Fedha taslimu hazipokelewi shuleni

## C. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria, kanuni na taratibu zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA kwa ujumla. Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima, tabia, kauli na vitendo hivyo. Wakati wote akiwa mwanafunzi kijana wako anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa shughuli za shule.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote anapokuwa shuleni.
h) Kutunza mali za umma, kuharibu mali ya umma kwa makusudi nikosa ambalo linaweza kumfukuzisha shule.
i) Hairuhusiwi kwa mwanafunzi:
   (i) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya
   (ii) Kunyoa kipara
   (iii) Kumpiga mwenzake au kupigana
   (iv) Kutukana
   (v) Kutia dawa nywele na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa.
   (vi) Kuvaa mapambo kama vile mikufu, bangili, rozali, tasbihi, kofia na vilemba
   (vii) Kuchomoa shati
   (viii) Kuvaa sketi chini ya kiuno (mlegezo)
   (ix) Kuvaa nguo za mitindo
j) Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma
k) Awe mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyosababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa darasani, maktaba, maabara, wakati wa kujisomea, paredi, bwenini au mikusanyiko yoyote.
l) Mwanafunzi ahudhurie vipindi darasani na kufanya kazi zote kama ilivyopangwa.
m) Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni bila kibali cha mkuu wa shule
n) Mwanafunzi hapaswi kuvaa mavazi ya nyumbani mara zote awapo shuleni
o) Hairuhusiwi kumiliki simu au kitu chochote cha kielektronik ***isipokuwa saa na calculator.***
p) Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na shughuli za kisiasa akiwa shuleni.
q) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia au kufika maeneo yafuatayo bila ruhusa maalum:
   (i) Ofisi za walimu
   (ii) Bohari za shule
   (iii) Maabara
   (iv) Nyumba za wageni (Guest house)
   (v) Nyumba za walimu/watumishi
   (vi) Mahali panapouzwa vilevi kama vile baa na vilabuni na magenge ya wahuni.
   (vii) Kwenye ngoma, disco, mziki na sherehe yoyote nje na ndani ya shule bila ruhusa maalum

## <u>MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI</u>

a) Wizi
b) Uasherati
c) Kutoa lugha ya matusi
d) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupiga au kupigana
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau **Bendera ya Taifa** sanjari na **Wimbo wa Taifa**
h) Kupata au kusababisha ujauzito
i) Kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu au jamii inayotuzunguka.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi au kifaa cha simu
n) Kufanya kosa la jinai

**KARIBU SANA MOHORO SEKONDARI**

**……………………**

**<u>SALUM B MPELA</u>**

**MKUU WA SHULE**

## D. MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

- Jina la mwanafunzi……………………………………………ADM No….……
- Kidato…………...……Mchepuo…………………….…mwaka…………………
- Uraia ………………..…… Dini……………………Dhehebu ……………………
- Tarehe ya kuzaliwa……………………Mahali alipozaliwa……………………….
- Nambari ya cheti cha kuzaliwa…………………………………………………….
- Tarehe ya kujiunga na shule ya Sekondari MOHORO……………………………
- Shule ya sekondari aliyotoka mwanafunzi ni………………………………………
- Kama ni mlemavu taja aina ya ulemavu……………………………………………
- Je unarudia kidato?......................kwa nini?.....................................................
- Bweni alilopangiwa…………………………………………………………………
- Anwani ya kudumu ya nyumbani kwa mwanafunzi S. L P ………………………
- Kijiji……………………Namba ya nyummba……………….Kata……………….
- Tarafa …………….Wilaya………………………Mkoa…………………………
- Simu ya nyumbani…………………………………………………………………..

  BABA:
  - Jina la baba……………………………………………………………………..
  - Je yu hai?.........................................................................................
  - Anwani yake ya sasa ni S L P …………………………………………..
  - Kazi yake……………….Dini yake………………. Dhehebu……………..
  - Je baba na mama wanaishi pamoja?.......................................................
  - Simu ya baba…………………………… simu ya kazini…………………..

    MAMA:
    - Jina la mama……………………………………………………………
    - Je yu hai?.........................................................................................
    - Anwani yake ya sasa ni S L P ………………………………………
    - Kazi yake…………….Dini yake……………. Dhehebu……………..
    - Mwajiri wa mama……………….......................................................
    - Simu ya mama…………………….. simu ya kazini…………………

      MLEZI
      - Jina la mlezi……………………………………………………
      - Uhusiano na mwanafunzi…………………………………………
      - Anwani yake ya sasa ni S L P ………..…………………………
      - Kazi yake…..…………..Dini yake……..… Dhehebu……………..
      - Mwajiri wa mlezi………..........................................................
      - Simu ya Mlezi…………………….. simu ya kazini………………

NDUGU WENGINE (Pasiachwe wazi)

PICHA

JINA………………………………UHUSIANO…………………SIMU……………………

PICHA

JINA………………………………UHUSIANO………………..SIMU………………………

PICHA

JINA………………………………UHUSIANO…………………SIMU……………………

PICHA

JINA………………………………UHUSIANO………………….SIMU……………………

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………tarehe……………………………..…………

KISWAHILI

Kila mwanafunzi aliyepangwa kuja kusoma somo la Kiswahili anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Kiswahili Kidato cha Tano na Sita (Taasisi ya Elimu Tanzania)
- Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 (Kilangi Enock)
- Tafsiri na Ukalimani (Mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) Lazima aje nayo Vile vile mwanafunzi anayesoma Kiswahili anapaswa kuja na vitabu vya RIWAYA viwili,MASHAIRI viwili na TAMTHLIYA viwili (**Chagua hapo chini kwenye orodha)**

**USHAIRI**

- Kimbunga (Haji Gora)
- Mapenzi Bora (Shabani Robert)
- Chungu Tamu (Theobald A Mvungi)
- Fungate ya Uhuru ( Mohamedi S Khatibu)

**RIWAYA**

- Usiku utakapokwisha (Mbunda Msokile)
- Kufikirika (Shabani Robert)
- Mfadhiri ( Hussein Tuwa)
- Vuta N Kuvute (Shafi Adam Shafi)

**TAMTHILIYA**

- Kwenye ukingo wa Thim (Ebrahim Hussein)
- Morani ( Emmanuel Mbogo)
- Nguzo Mama (Penina Mhando)
- Kivuli kinaishi (Said Mohamed)

**PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**RUFIJI DISTRICT COUNCIL**

**MOHORO SECONDARY SCHOOL**

## E. MEDICAL EXAMINATION FORM

To the medical officer ……………………………………………………………
Please examine …………..……………………………….as student in the following areas:-

- Eye sight…………………………………….…………………………………
- Hearing …………………………….………………………………………..
- Speech ………………………………………………………………………
- Specimen:
    - Stool ………..……………………………………………………
    - Urine.………..……………………………………………………..
    - Blood ……………………………………………………………..
- Athma/tuberculosis.………..……………………………………………………
  ……………………….…………………………………………………………
  ……………………..……………………………………………………………
- Pregnancy……………………………………………………………………
- Hereditary diseases e.g. Diabetes, epilepsy, Sickle Cell Anaemia ……………………………………………………………..……………………
- Any disability to be reported…………………………………………………………
- Other diseases…………………………………………………………..

……………………

SALUM B MPELA

HEAD MASTER

**Medical certificate**

I have examined the above student; she/he is physically fit/unfit as a student.
Reason ……………………………………………………………………………….

Medical officer's name …………………… Designation.………….….. Signature……………

Station………………………………Date …………………………Official stamp……..……